**Ili kupata chanjo ya ugonjwa wa Kideri iliyopendekezwa, wasiliana na wadau wetu kama ifuatavyo:**

Dk Sultan Jaribu Hussein
Mshauri-Mwelekezi wa miradi ya
ND kanda ya Kati na Kaskazini Tanzania
Simu: +255784681144

Dk Charles Samwel Ndesamburo
Chasa - Morogoro Tanzania
Mtaa wa Ngoto, Nyumba Na. 26
S.L.P. 1883 Morogoro, Tanzania.
Simu: (+255) 768 580442

Dk Nderingo Elisante Ngowi
PHARMAVACS LTD
Simu: +255784918504

GALVmed inafadhiliwa na
Bill & Melinda Gates Foundation na Serikali ya Uingereza

BILL & MELINDA GATES foundation

UKaid
from the British people




# CHANJA KUKU WAKO DHIDI YA UGONJWA WA KIDERI (MDONDO)

## Kideri ni ugonjwa wa namna gani?

Ugonjwa wa Kideri (ama wengine huuita Mdondo) ni ugonjwa wa ndege wenye kuambukiza kwa kasi, ambao huathiri jamii nyingi za ndege wafugwao kama kuku, kanga na ndege wengine. Ugonjwa wa Kideri unaweza kuua kundi lote la ndege uliowafuga ikiwa hawajachanjwa dhidi ya ugonjwa huo na ukitokea mlipuko wa ugonjwa huo, unaweza kuteketeza kuku wote kijijini mwako na hata vijiji vya jirani. Kwa hivyo, ni muhimu kuchanja kundi lako la ndege/kuku!

Dalili zinazoweza kukuonesha kuwa kuku wako wana ugonjwa wa Kideri

## Dalili za ugonjwa wa Kideri hutofautiana kutegemeana na:

- Aina ya virusi
- Aina ya ndege/kuku
- Umri na afya ya ndege/kuku
- Hali ya mazingira
- Eneo gani la mwili lilikoshambuliwa na virusi vya kideri.

Kutokana na sababu zilizoorodheshwa hapo juu, hakuna dalili mahsusi za ugonjwa wa Kideri, lakini kuna dalili ambazo unaweza kuzitazama ikiwa una shaka kuwa kuku wako wanaugua ugonjwa wa Kideri:

- Vifo vya ghafla bila kuonesha dalili zozote
- Kuvimba kwa kichwa na shingo
- Kuharisha uharo wa kijani
- Utagaji wa mayai kushuka kwa kiasi kikubwa au kusimama kabisa
- Kutetemeka, kichwa kugeuzwa upande mmoja,
- Kupooza kwa mabawa na miguu

Vifo vingi katika kipindi kifupi Hata hivyo, inapofikia muda unagundua dalili hizo, unakuwa tayari umeshachelewa mno! Ndio maana inashauriwa kuchanja ndege/kuku wako kila mara.

## Ugonjwa wa Kideri hueneaje?

Ugonjwa wa Kideri huambukizwa kwa kiwango kikubwa mno na huenea kwa kuku wengine kwa kasi kubwa ndani ya muda mfupi sana. Ugonjwa huenezwa kwa njia ya kinyesi na hewa. Unaweza kuenea pia kupitia:

- Maji ya kunywa yaliyobeba virusi
- Kugusa chakula kilichobeba virusi
- Kugusa kuku wagonjwa
- Kugusa vitu au mazao yaliyobeba virusi na kuku wagonjwa (nyama ya kuku, matumbo, mayai na manyoya)
- Kugusana na watu au vyombo kutoka katika maeneo yaliyoathiriwa na ugonjwa (viatu, nguo, na matairi ya gari, ambavyo vyote vinaweza kubeba virusi vya ugonjwa)
- Nyumba za kuku zenye virusi


## Kuzuia ugonjwa wa Kideri kwa njia ya chanjo

Kuchanja kuku wako dhidi ya ugonjwa wa Kideri ndio njia bora ya kuzuia kuku/ndege wako wasipate ugonjwa huo. Iwapo kuku/ndege hawajachanjwa, wanaweza kuugua ugonjwa wa Kideri. Ikiwa wataugua ugonjwa huo, hawawezi kutibiwa au kupona.



## Utachanjaje kuku/ndege wako dhidi ya ugonjwa wa Kideri

- Pata chanjo kutoka wakala mzuri. Chanjo inayopendekezwa ni Chanjo ya Kideri I-2 (I-2 Newcastle vaccine). Kuna wazalishaji wengi wa Chanjo ya Kideri I-2 wakitumia majina mbalimbali ya kibiashara, lakini ni muhimu kuthibitisha kuwa unachonunua ni chanjo ya I-2.
- Kamata kuku kwa uthabiti huku ukiwaegemeza upande
- Weka tone moja la chanjo ya I-2 kwenye jicho moja ikiwa unawachanja kupitia machoni. Iwapo unawachanja kupitia puani, hakikisha kwanza unazisafisha pua.
- Dondoshea tone moja jichoni na subiri kuku achezeshe kope AU dondoshea tone moja puani na msubiri kuku avute hewa.



Weka tone la maji kwenye jicho kisha subiri mpaka kuku wako apepese jicho

## Kumbuka!

- Chanja kila baada ya miezi mitatu kwa kuku wa umri WOTE.
- Chanja kuku wenye afya tuu. Chanjo si kwa ajili ya kutibu au kuponyesha.
- Epuka kuweka chanjo katika mazingira ya kiwango cha juu cha joto na jua la moja kwa moja
- Chanjo ya Kideri I-2 (I-2 Newcastle vaccine) huwalinda kuku dhidi ya ugonjwa wa Kideri pekee
- Lisha kuku wako vizuri
- Iweke nyumba ya kuku katika hali ya usafi na bila vijidudu daima. Nyumba inatakiwa kuwa na hewa ya kutosha na ikiwa imeinuliwa ili kinyesi na taka zingine ziweze kudondoka kwenye udongo pasipo kuchafua chakula au maji.
- Weka eneo lenye dawa ya kuchovya miguu mlangoni pa nyumba ya kuku ili kuua vijidudu na virusi miguuni mwako kila mara uingiapo
- Weka nyumba ya kuku mbali na zile za binadamu na wanyama wengine ili kuzuia kuenea kwa magonjwa
- Safisha vyombo vya kulishia kuku na kunyweshea kwa kutumia maji vuguvugu yenye sabuni na badilisha chakula na maji kila siku.

## Njia nyingine za kudhibiti ugonjwa wa Kideri

Iwapo kuku wako wameshaugua ugonjwa:

- Chinja kuku wako wagonjwa wote mapema iwezekanavyo. Inashauriwa kuchoma kuku wako wagonjwa na waliokufa hadi wawe majivu kabisa au kuzika kuku waliokufa, manyoya na matumbo yao katika kina kirefu cha udongo.
- Usiuze au kuwapa watu kuku wagonjwa, kwani kitendo hicho kinaeneza ugonjwa
- Usichanje iwapo kijijini kwako tayari kuna mlipuko wa ugonjwa wa Kideri. Hadi hapo kuku wa mwisho akifa kwa ugonjwa, subiri angalau mwezi mmoja kabla kuleta kuku wapya.
- Punguza kukutana kwa kuku, bata, njiwa, na kanga
- Kwa kuku wenye afya, walishe pumba za mahindi, mbegu za nafaka, majani, wadudu na minyoo. Hii itasaidia kuku kuwa na afya bora na kukua haraka.
- Tafadhali muone afisa mifugo au wasaidizi wa afya ya mifugo mara unapobaini dalili za ugonjwa au kupungua kwa uzalishaji wa mayai.